

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

634

STADI ZA KAZI

Muda: Saa 3

Mwaka : 2021

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vyote vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha aina nne za vifani vinavyotokana na ususi na kwa kila kimoja taja matumizi yake.
2. Kwa kutumia hoja nne, ainisha umuhimu wa kuzingatia urari wa kijinsia katika ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi.
3. (a) Nini maana ya shairi?
(b) Eleza kwa kifupi vipengele vitatu muhimu vya kuzingatia wakati wa kutunga shairi.
4. Elezea kwa kifupi manufaa ya mbinu ya ziara katika kufundishia mada ya *Upigaji picha* kwa wanafunzi wa Darasa la Sita. Toa hoja nne.
5. Kwa kutumia mifano, tofautisha kati ya kushona na kutarizi.
6. Bainisha vigezo vinne vinavyoweza kutumika katika kuchagua mbinu ya kufundishia mada ya *Ufundi* kwa wanafunzi wa Darasa la Tano.
7. Eleza kwa kifupi mambo manne anayotakiwa kuyafanya mwanafunzi ili aweze kuimba solfa vizuri.
8. Toa maana ya upambaji nguo kwa mafundo na taja nguo nne zinazoweza kupambwa kwa njia hiyo.
9. (a) Nini maana ya dhana biashara ndogondogo?
(b) Elezea kwa kifupi, aina tatu za biashara ndogondogo.
10. Fikiria unafundisha mada ndogo ya *Ufugaji bora wa kuku wa kienyeji* kwa wanafunzi wa Darasa la Tano, ni sifa zipi za kuku wa kienyeji utakazowafundisha wanafunzi wako? Toa sifa nne.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Ufuaji wa nguo ni stadi inayofuata kanuni mbalimbali katika utekelezaji wake. Kwa kutumia hoja tano, fafania kanuni hizo.
12. Eleza mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutengeneza juisi ya matunda. Toa hoja tano.

13. Fikiria unaandaa nukuu za somo kuhusu dhana ya *Ustawishaji wa mboga*, chambua hatua sita za kustawisha mchicha shambani.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. (a) Chambua sehemu kuu mbili za Muhtasari wa somo la Stadi za Kazi.
- (b) Kwa nini mwalimu anatakiwa kufanya uchambuzi wa Muhtasari kabla ya kufundisha? Eleza kwa kutoa hoja nne.
15. Kwa kutumia hoja tano, eleza namna utakavyowafundisha wanafunzi kupiga ala sahili za muziki.
16. Kwa kutumia hoja sita, fafania umuhimu wa kutathmini matokeo ya upimaji katika somo la Stadi za Kazi.